# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI - AFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

**MWL. HAROUN ALI SULEIMAN (MBM)**

# KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

***ZANZIBAR***

***MEI, 2022***

# YALIYOMO


**YALIYOMO** ........................................................................................................ i

**A.** ........................................................................ **UTANGULIZI** 1

**B.MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022** ........................................................................ 5

G01 - Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ............ 7

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria ................................ 8

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini ................................ 10

Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora ................................ 12

Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma ............ 13

Programu ya Huduma za Serikali Mtandao. ................................ 16

**Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora** ........................................ 18

Uratibu wa Usimamizi wa Programu za Miradi ya Wizara .................. 20

Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma kwa Awamu ya Pili ........................................................................ 22

Programu ya Uratibu wa ARKSUUB - Pemba ................................ 23

**TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU.** ........................................ 24

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ................................ 24

Chuo cha Utawala wa Umma ........................................ 24

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ................................ 26

Skuli ya Sheria Zanzibar ........................................ 28

**G02: MAHKAMA KUU** ........................................ 30

Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki ................................ 30

**G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU** ........................................ 33

Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa huduma za Sheria ...................... 33

**G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**........ 35

Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai ........ 35

**G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA**........ 37

Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria ........ 37

**E04: OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**........ 39

Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa fedha na Rasilimali za Umma ..... 39

**EO5: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI** .. 41

Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi........ 41

**E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA**........ 43

Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma........ 43

**E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**........ 44

Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini ........ 44

**C.MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023** .... 45

**D.VIPAUMBELE VYA OFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**... 46

Malengo Makuu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ........ 47

**G01: AFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**........ 50

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria........ 50

Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora........ 51

Programu ya Uendelezaji wa Watumishi wa Umma. ........ 52

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ARKSUUB........ 54

**TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU- G01**........ 57

Chuo Cha Utawala wa Umma ........ 57
Skuli ya Sheria Zanzibar ........ 58
**G02: MAHKAMA KUU** ........ 58
Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki ........ 58
**G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU** ........ 59
Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa huduma za Sheria ........ 59
**G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA** ........ 60
Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai ........ 60
**G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA** ........ 61
Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria ........ 61
**G14: OFISI YA MUFTI MKUU ZANZIBAR** ........ 62
Programu ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masula ya Kiislamu . 62
**G12: KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA** ........ 63
Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Mirathi, Zakka na Misaada.. 63
**G13: WAKALA WA SERIKALI MTANDAO** ........ 64
Programu ya Huduma za Serikali Mtandao ........ 64
**G15: TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA** ........ 65
Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi ........ 65
**E04: AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI** ........ 66
Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma..... 66
**E05: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI** ........ 66
Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi....... 66

**E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA** ........ 67

Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma ........ 67

**E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI** ........ 69

Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini ........ 69

**E. SHUKRANI** ........ 70

**F. HITIMISHO** ........ 70

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati, ili liweze kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii kwa ajili ya kuwasilisha taarifa ya utelekezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 na mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutuwezesha kutekeleza vyema mipango na malengo tuliojipangia ya kuwahudumia wananchi na kuimarisha shughuli za utoaji wa haki.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa

umahiri wake katika kuiongoza Zanzibar na kuendelea kutekeleza ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa Uchaguzi Mkuu na nyakati mbali mbali kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu, afya njema na umri mrefu Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kuiongoza Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa ufanisi na mafanikio makubwa tangu aliposhika madaraka ya Urais. Sote tumeshuhudia utekekelezaji mzuri wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 kama yalivyoasisiwa na mtangulizi wake Hayati John Pombe Joseph Magufuli.

5. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa uongozi wake mzuri na namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya kuingoza nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika,** niruhusu pia nimpongeze Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalla, makamo wa Pili wa Rais, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali katika Baraza lako Tukufu na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya CCM hapa Zanzibar.

7. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi na kupelekea kufanya kazi na Ofisi yangu kwa mara nyengine tena katika nafasi ya Mwenyekiti kama ilivyokuwa katika Baraza lililopita. Uteuzi wake huo unaonyesha wazi uwezo alionao katika kufanya kazi za kuongoza na kusimamia Kamati za Baraza na imani kubwa uliyonayo Mheshimiwa Spika, juu yake. Aidha, naomba nimpongeze Makamo Mwenyekiti Mheshimiwa Mtumwa Peya Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Bumbwini na Wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo na mashirikiano mazuri waliotupatia katika kukamilisha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 inayoendelea na kuongeza ufanisi wa utekelezaji kama itakavyoelezwa katika hotuba hii.

8. **Mheshimiwa Spika,** naomba kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru aliekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Welezo, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Afya alivyosaidia Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wakati wa uongozi wake. Pia, nawapongeza Mawaziri wote waliopata uteuzi pamoja na Manaibu Mawaziri wapya.

9. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza pia, Mheshimiwa Juma Ali Khatib, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa mashirikiano yao mazuri wanayoipatia Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

10. **Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa pongezi zifuatazo: kwanza kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Naibu wako na Wenyeviti wa Baraza kwa kuendelea kuliongoza Baraza letu kwa umahiri na uvumilivu mkubwa na kusimamia kanuni tulizojiwekea. Pili, Mawaziri wenzangu na Wawakilishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya na ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Tatu na mwisho, lakini si kwa umuhimu napenda kuipongeza na kuishukuru familia yangu na wapiga kura wa Jimbo la Makunduchi

ambao wameendelea kunionyesha upendo na ushirikiano mkubwa hata pale ninapokuwa nimebanwa na majukumu ya kitaifa nje ya Jimbo langu la uchaguzi. Nawaahidi kuendelea kushirikiana nao katika kulileletea maendeleo Jimbo letu na nchi yetu kwa jumla.

11. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naomba kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2021/2022, na mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2022/2023 kama ifuatavyo.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imesimamia jumla ya mafungu 10 ya bajeti yaliotekelezwa kupitia program kuu 15 ambayo ni; **G01 -** Ofisi Kuu; **G02-** Mahkama Kuu; **G03**- Afisi ya Mwanasheria Mkuu; **G04**- Mkurugenzi wa Mashtaka na **G05**- Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na fungu **A02**- Afisi ya Rais Baraza la Mapinduzi. Afisi pia, inasimamia mafungu **E04**- Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na **E05**-Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; **E07**- Kamisheni ya Utumishi wa Umma; na **E08** Tume ya Utumishi Serikalini. Vile vile, Afisi hii imesimamia ruzuku ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Tume ya Maadili

ya Viongozi wa Umma, Chuo Cha Utawala wa Umma (IPA) na Skuli ya Sheria Zanzibar.

13. **Mheshimiwa Spika,** mabadiliko madogo ya Wizara za Serikali yaliofanywa katika mwaka wa fedha **2021/2022**, yamepelekea fungu **A02** - Afisi ya Rais Baraza la Mapinduzi kuhamishiwa Ofisi ya Rais, Ikulu pamoja na bajeti za Idara ya Usalama wa Serikali (GSO) na Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za taifa zilizokuwemo kwenye fungu **G01**.

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2021/2022**, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ilipanga kutumia jumla ya Shilingi **60,312,975,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo, shilingi **37,631,800,000** zilipangwa kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi **22,681,175,000** zilipangwa kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya mafungu ya bajeti yaliotokana na mabadiliko ya Wizara, jumla ya Shilingi **2,194,500,000** kutoka kwenye fungu **A02** zilihamishiwa Afisi ya Rais, Ikulu.

15. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na mabadiliko hayo, makadirio ya bajeti ya Ofisi kwa mwaka **2021/2022**, ni Shilingi **58,118,475,000** kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi **35,437,300,000** ni matumizi ya

kawaida na Shilingi **22,681,175,000** ni kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia mwezi machi **2022**, jumla ya Shilingi **20,552,068,545** zimepatikana sawa na asilimia **54.61** kwa matumizi ya kawaida.

Kwa upande wa kazi za maendeleo, hakuna fedha zilizoombwa kutoka Serikalini kutokana na uamuzi wa Serikali wa kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kupitia Mpango wa Ujenzi wa Majengo ya Serikali.

Pia, Ofisi ilikusanya Shilingi **715,377,937.20** kupitia vyanzo vya mapato yake na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na Shilingi **1,137,136,400** zimekusanywa kupitia Chuo cha Utawala wa Umma (**angalia viambatanisho nam. 1c**).

Taarifa za makadirio ya fedha na matumizi halisi kwa kila fungu na program zilizomo katika Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora zitaonekana katika mafungu ya taasisi hizo kupitia program husika.

### *G01 - Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora*

16. **Mheshimiwa Spika,** Fungu **G01** linahusisha Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria; Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora;

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini; Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma; Programu ya Huduma za Serikali Mtandao; na Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa ARKSUUB.

17. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya Shilingi **12,027,975,000** zilipangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya program za fungu ***G01.*** Hadi kufikia mwezi Machi **2022,** jumla ya Shilingi **5,717,743,139** zimepatikana sawa na asilimia **47.53** ya bajeti kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na matumizi mengineyo ya fungu **G01**. (**angalia kiambatanisho nam. 1a).**

18. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2022, hatua za utekelezaji wa programu za Fungu **G01** na fedha zilizopatikana ni kama ifuatavyo:-

### *Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria*

19. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Msaada wa Kisheria kupitia program hii imetoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi na taasisi mbali mbali na vyuo vikuu kupitia maadhimisho ya wiki ya msaada wa sheria, mkutano wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia na mikutano ya wazi iliofanyika katika maeneo mbali mbali. Jumla ya wananchi 4,053 wa Shehia 16 za Pemba na

Shehia 20 za Unguja walifikiwa na kupatiwa elimu hiyo. Idara imewajengea uwelewa Maofisa wa Jeshi la Polisi na Ustawi 160 kuhusu msaada wa kisheria, kuandaa jukwaa la mwaka la Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria na kuandaa mikutano ya robo mwaka ya msaada wa kisheria.

Idara pia, imetoa mafunzo ya siku mbili (2) ya kuwajengea uwelewa Waheshimiwa Majaji, Mahakimu na Makadhi 64 wa Unguja na Pemba juu ya upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa watu wasiokuwa na uwezo na wenye mahitaji maalum Mahakamani.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Idara imeandaa Mkutano na Maafisa Waandamizi wa Chuo cha Mafunzo na Jeshi la Polisi wa kujadili utayarishaji wa Muongozo wa Upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa watu waliopo vizuizini. Aidha, Idara inaendelea na matayarisho ya Muongozo wa Upatikanaji wa Msaada wa Kisheria na Muongozo wa Uanzishwaji wa Vituo vya Msaada wa Kisheria katika Vyuo Vikuu na Vituo vya Mafunzo ya Sheria.

Vile vile, Idara imechapisha na kusambaza katika taasisi husika nakala 100 za Kanuni za Malipo ya Wakili na Vakil, nakala 250 za Muongozo wa Uratibu wa Huduma za Msaada wa Kisheria katika Serikali za Mitaa, nakala 650 za Tafsiri ya Ripoti ya Hali Halisi ya Msaada

wa Kisheria na ripoti ya mwaka ya msaada wa kisheria.

21. **Mheshimiwa Spika,** program hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **204,070,000** na hadi kufikia mwezi Machi **2022**, jumla ya Shilingi **89,278,110** zimepatikana sawa na asilimia **43.7** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

### *Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini*

22. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar imeanzishwa rasmi kupitia Sheria Namb. 4 ya mwaka 2021, kwa ajili ya kusimamia uendeshaji wa masuala ya Kiislamu hapa Zanzibar.

Katika kipindi hiki, Ofisi imesajili kwa mujibu wa Sheria jumla ya Misikiti 115 na Madrasa 321 na kufanya ukaguzi wa Misikiti 104 na Madrasa 235 na kutoa ushauri wa kuendeleza taasisi hizo. Aidha, mafunzo ya ualimu kwa Walimu wa Madrasa yametolewa kwa Walimu 362 na kupewa Shahada na Leseni za ualimu. Kati ya hao, Walimu 259 ni wanaume na 103 ni wanawake. Lengo la mafunzo hayo ni kupata Walimu wenye taaluma ya ufundishaji na maadili katika kazi zao.

Ofisi pia, imewapatia mafunzo ya kupinga udhalilishaji katika Madrasa za Quran viongozi wa Dini ya Kiislamu na Walimu wa Madrasa 50

na kuendelea na mafunzo ya ualimu kwa Walimu wa Madrasa 150 kwa upande wa Unguja katika Msikiti wa Jamiu Zinjibar.

23. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya Wanandoa 553 (wanawake 380 na wanaume 173) wamehitimu mafunzo ya maadili ya ndoa yenye lengo la kupunguza talaka na migogoro ya ndoa. Ofisi imepokea na kushughulikia migogoro 447 ya kifamilia, ndoa na mirathi na kutatua migogoro tisa (9) ya Misikiti na Madrasa kati ya 22 iliopokelewa katika kipindi hicho. Migogoro mitatu (3) inaendelea kushughulikiliwa.

Vile vile, Ofisi imefanya kikao cha Baraza la Ulamaa na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Dini ya Kiislamu kupitia vyombo vya habari, kuandaa na kurusha hewani vipindi vya mawaidha ya Dini ya Kiislamu na kujibu masuali 180 yalioulizwa kupitia vipindi hivyo.

24. **Mheshimiwa Spika,** suala la upatikanaji wa taarifa za kuandama kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwa wakati ni muhimu sana na linasaidia kupunguza khofu juu ya kuonekana kwa mwezi muandamo miongoni mwa Waislamu. Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar imepokea kifaa maalum cha kutizamia mwezi kutoka Ubalozi wa Oman kwa ajili ya kufanikisha jambo hilo. Ofisi inawaomba Waislamu wote nchini kuendelea kufuatilia taarifa za kuandama kwa mwezi zinazotolewa na Ofisi ya Mufti Mkuu kwa

ajili ya kusaidia kutekeleza vyema Ibada ya funga katika mwezi Mtukufu wa Ramadhan na kufungua katika mwezi wa Mfunguo Mosi kwa wakati sahihi.

25. **Mheshimiwa Spika,** program hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **879,095,000** na hadi kufikia mwezi Machi **2022,** jumla ya Shilingi **623,953,600** zimepatikana sawa na asilimia **70.9** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

### *Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora*

26. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi **2022**, Idara ya Utawala Bora imetayarisha Jarida la Utawala Bora linalotolewa kila mwaka, kuadhimisha siku ya Maadili na Haki za Binaadamu Unguja na Pemba na kuandaa kongamano la kitaifa la utawala bora kwa kushirikiana na taasisi za Utawala Bora. Idara imekamilisha zoezi la tathmini ya kuangalia utekelezaji wa majukumu ya kijamii kwa Wawekezaji katika mradi wa makaazi ya kisasa Fumba na kuandaa Mswada wa Sheria ya Kusimamia Majukumu ya Jamii baada ya kukamilika zoezi la ukusanyaji wa maoni ya wahusika mbali mbali.

Aidha, elimu ya utawala bora ya kuelimisha jamii kuhusu masuala ya rushwa na uwajibikaji imetolewa kupitia matangazo mafupi mawili (2) na vipindi 58 vya Utawala Bora na maelezo baada

ya habari 10 vilivyotayarishwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar, Redio Jamii Mkoani na Micheweni Pemba.

27. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **253,317,443**. Hadi kufikia Machi 2022, Shilingi **134,861,585** zimepatikana sawa na asilimia **53.2** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

### *Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma*

28. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Idara ya Mipango ya Rasilimaliwatu kupitia program hii imesimamia utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu wa mwaka 2022/2023, katika utumishi wa umma na kufanya vikao vya majadiliano na Taasisi za Umma kubainisha watumishi waliopo katika Utumishi na mahitaji ya nafasi mpya zinazohitajika katika Utumishi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Idara imefanya mapitio ya mkataba wa ajira katika utumishi wa umma na kuandaa muongozo wa ubadilishaji wa kada za watumishi wa umma.

29. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeandaa Sera ya Mafunzo kwa Watumishi wa Umma ya mwaka 2022, pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Sera hiyo na kuratibu fursa 42 za mafunzo ya watumishi wa umma nje ya nchi zinazotolewa

na Washirika wa Maendeleo kwa watumishi wa Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea. Jumla ya Watumishi 32 waliomba kupatiwa nafasi za mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Uzamili na watumishi 20 wameomba nafasi za mafunzo ya muda mfupi katika fani ya Ukaguzi (Public Audit) kupitia ufadhili wa Jamhuri ya Watu wa Korea. Maombi hayo tayari yamewasilishwa Ubalozi wa Korea na hatua za uchambuzi wa maombi hayo zinaendelea.

Aidha, Idara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeandaa mapendekezo ya kurejesha utaratibu wa kuwapatia mikopo ya elimu ya juu watumishi wa umma kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu kwa ajili ya kuwawezesha watumishi wa umma kujiendeleza kitaaluma. Idara pia, imeratibu mafunzo ya wastaafu katika utumishi wa umma na kutoa vibali vya uhamisho wa watumishi 105 kutoka taasisi mbali mbali za Serikali wenye lengo la kuimarisha utendaji katika utumishi wa umma.

30. **Mheshimiwa Spika,** uhakiki wa Watumishi wa Umma katika Wizara na Taasisi zote za Serikali unaendelea. Lengo la uhakiki huu ni Serikali kutaka kujua idadi halisi ya watumishi waliopo katika Taasisi za umma, namna walivyopangwa na mahitaji halisi ya watumishi katika utumishi wa umma ili kuhakikisha matumizi sahihi ya rasilimaliwatu kwenye taasisi hizo. Uhakiki huu unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2022.

31. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **338,261,000** na hadi kufikia Machi **2022**, jumla ya Shilingi **190,020,900** zimepatikana sawa na asilimia **56.2.**

32. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi kupitia programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi imefanya mapitio ya kazi na majukumu ya Wizara na Taasisi za Serikali, uhakiki wa mishahara na Maposho katika Wizara na Taasisi za Serikali na kupendekeza viwango vya mishahara Serikalini kwa mazingatio.

    Idara imetoa Matoleo na Miongozo mitatu (3) ya kiutumishi kuhusu mtumishi aliyeko kwenye kipindi cha majaribio, malipo ya mafao ya kumaliza muda wa mkataba wa ajira ya muda mfupi na muongozo kuhusu madai ya malipo baada ya kumalizika mikataba kwa wafanyakazi wenye ajira ya mkataba baada ya kustaafu.

    Aidha, Idara imekamilisha mapitio ya miundo 17 ya Wizara za SMZ na tayari imeshajadiliwa katika vikao vya Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

33. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **350,977,868.78** na hadi kufikia Machi **2022**, Shilingi **242,502,310** zimepatikana sawa na asilimia **69** kwa matumizi ya mshahara na matumizi mengineyo.

### *Programu ya Huduma za Serikali Mtandao.*

34. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali Mtandao kupitia programu hii imetoa miongozo minane (8) ya uandaaji wa nyaraka za TEHAMA kwenye Taasisi za Umma na kuidhinisha maombi 11 ya ununuzi wa mifumo na vifaa vya TEHAMA katika taasisi za Serikali. Aidha, Wakala imefanya mapitio ya nyaraka za kitaalamu tano (5) za ununuzi na uanzishaji wa mifumo pamoja na kusimamia na kushauri utekelezaji wa miradi mitano (5) ya utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA katika Utumishi wa umma kama ifuatavyo: Mfumo wa bajeti na matumizi ya Serikali (BAMAZ), Mfumo wa usimamizi wa taarifa za watumishi na mishahara (Integrated Human Resource and Payroll System); Mfumo wa Usimamizi wa Ajira za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (Ajira Portal); Mfumo wa Ununuzi kwa njia ya Kieletroniki (e-Procurement); na Mfumo wa Huduma za Jamii ya Afya Zanzibar (Bima ya Afya Zanzibar).

35. **Mheshimiwa Spika,** Wakala imesimamia Mfumo wa ZanMalipo ambao tayari umeanza kutumiwa na taasisi 20 na kutoa mafunzo ya matumizi ya Mfumo huo kwa watendaji husika wa Taasisi zote za Umma ili kuwajengea uwezo watendaji wa Taasisi hizo kuelewa madhumuni ya uanzishwaji wa mfumo huo na mahitaji ya vifaa vinavyohitajika. Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwasaidia watumiaji wa mfumo huo

kutengeneza Ankara kwa kuingiza taarifa sahihi za mteja, kutoa risiti kwa mteja aliefanya malipo ya huduma na kutoa msaada wa kiufundi kwa watumiaji.

Kwasasa Wakala inaendelea kuziunganisha Taasisi zinazotumia mifumo ya TEHAMA na mfumo wa Zanmalipo na jumla ya taasisi 14 tayari zimeshaunganishwa na mfumo huo kati ya 29 zilizoanza taratibu za kuunganishwa.

36. **Mheshimiwa Spika,** mifumo mbali mbali ya TEHAMA inayotumika na Taasisi za Serikali imekaguliwa katika kipindi hiki ili kuhakikisha usalama wa matumizi wa mifumo hiyo kwa wakati wote.

Vile vile, mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) na Mfumo wa baruapepe “GMS” yametolewa kwa Watendaji wa Taasisi za Umma ili kuhakikisha taratibu za kimasjala zinafanyika kimtandao kwenye Taasisi zote za Umma.

37. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **659,366,000**. Hadi kufikia Machi **2022**, Shilingi **451,657,175** zimepatikana sawa na asilimia **68.4** kwa matumizi ya mshahara na matumizi mengineyo.

### Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

38. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia programu ya Uongozi na Utawala imeendelea kuhudumia uendeshaji wa Ofisi, kusimamia masuala ya nidhamu na kulipa stahiki za watumishi. Idara imetekeleza kazi ya upimaji utendaji kazi kwa watumishi 65 na kuwapatia nyongeza ya mshahara baada ya kufaulu upimaji huo.

Kwa upande wa maslahi ya watumishi, jumla ya watumishi 112 wamelipwa stahiki zao za nyongeza ya mshahara, posho la likizo, malipo baada ya saa za kazi na malipo ya ubani wa kufiwa na watu wao wa karibu.

Aidha, Idara imeratibu na kuandaa vikao vinne (4) vya Kamati ya Uongozi kujadili na kuidhinisha nyaraka za kisera na kisheria zilizowasilishwa Serikalini, vikao 22 vya kupeana taarifa za utekelezaji wa majukumu ya kila wiki, 16 vya Bodi ya Zabuni kujadili zabuni za ununuzi wa vifaa na huduma mbali mbali na vikao vitatu (3) vya Kamati ya Ukaguzi na kuandaa ripoti.

39. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeandaa Mpango wa Rasilimali watu wa Mwaka 2022/2023 ili kutoa mahitaji halisi ya watumishi wa Wizara na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi saba (7). Pia, Watumishi 52 wamepatiwa

mafunzo mafupi ya utunzaji wa kumbukumbu, TEHAMA, Ofisi Mtandao na matumizi ya Mfumo wa Zanmalipo.

Vile vile, jumla ya habari 82 za matukio mbali mbali ya Wizara, Makala tisa (9) na vipindi 37 vimeandaliwa na kutolewa katika vyombo vya habari.

**40.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **1,794,136,000** na hadi kufikia Machi **2022**, jumla ya Shilingi **1,187,703,473** zimepatikana sawa na asilimia **66** kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

**41.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi **2022** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu na kusimamia mapitio na marekebisho ya Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao na Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma (IPA).

Aidha, Idara imeratibu na kuandaa nyaraka za kisera na kisheria zilizowasilishwa Serikalini na kutolewa uamuzi kama vile, nyaraka za mapendekezo ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Hijja na Ukusanyaji wa Zakka hapa Zanzibar. Idara imetayarisha Bajeti na Mpango wa mwaka

2022/2023, ripoti za utekelezaji za robo na nusu mwaka na kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2020/2025 kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 na Mpango wa Maendeleo wa 2021/2026.

Kwa upande wa utafiti wa Hali ya Rushwa na Utawala Bora ripoti ya utafiti huo imekamilika na kutarajiwa kuwasilishwa kwa wahusika kwa kutolewa maoni.

42. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **296,918,000**. Hadi kufikia Machi **2022**, Shilingi **158,952,215** zimepatikana sawa na asilimia **53.5** kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

### *Uratibu wa Usimamizi wa Programu za Miradi ya Wizara*

43. **Mheshimiwa Spika,** Idara kwa kushirikiana na taasisi husika imeratibu na kusimamia utekelezaji wa program za miradi kama ifuatavyo:

### *Program ya Mradi wa Uwezeshaji wa Kisheria na Upatikanaji wa Haki (LEAP).*

Mradi huu unaotekelezwa kupitia taasisi za Mahkama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Idara ya Msaada wa Kisheria ulitekelezwa

kuanzia mwezi Januari 2021 na kamilika mwezi Disemba 2021, kwa awamu ya kwanza chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la UNDP. Mradi umeongezwa muda wa miezi sita (6) ya ziada kuanzia mwezi Januari 2022 hadi Juni 2022, ili kukamilisha baadhi ya shughuli ambazo hazikutekelezwa katika kipindi cha mradi kilichomalizika pamoja na kuandaa mradi wa Uwezeshaji wa Kisheria na Upatikanaji wa Haki kwa awamu ya pili (LEAP II) na kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria wa Awamu ya Pili uliotayarishwa kupitia mradi huu na unaotarajiwa kutekelezwa kuanzia mwezi Julai 2022.

**44.** **Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **379,796,400** na umetumia Shilingi **367,085,710** sawa na asilimia 96. Aidha, katika kipindi cha nyongeza ya miezi sita kilichoanzia Januari 2022, na kumalizikia mwezi Juni 2022, jumla ya Shilingi **992,805,660** zimepangwa kutumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali za mradi.

**45.** **Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili la upatikanaji wa haki Idara imeratibu na kufuatilia upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa program ya mradi wa upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana kuhusu masuala ya udhalilishaji kupitia ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughikia Wanawake (UN Women) na Shirika la Maendeleo la

Ujerumani (GIZ). Taratibu za upatikanaji wa fedha katika Mashirika hayo zinaendelea.

### *Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma kwa Awamu ya Pili*

46. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefuatilia upatikanaji wa msaada wa kitaalamu na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa baadhi ya shughuli ziliomo katika Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma kwa Awamu ya Pili katika Benki ya Dunia na UNDP. Kupitia programu hii rasimu ya Mradi wa Kuharakisha utoaji wa huduma katika utumishi wa umma (Accelerated Public Service Delivery Program- APSDP) inayotekelezwa kwa pamoja baina ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya SMT na Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma Zanzibar chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la UNDP tayari imeshaandaliwa.

Aidha, matayarisho ya utafiti wa kina wa kuangalia usimamizi na uendeshaji wa utumishi wa umma Zanzibar (Diagnostic Study to Enhance Public Service Governance) kupitia msaada wa kitaalamu wa Benki ya Dunia yanaendelea vyema kwa kutayarisha hadudi za rejea na uteuzi wa wataalamu wa kufanya za kazi hiyo. Utafiti huo unatarajiwa kuanza mapema mwezi Mei 2022 na kukamilika mwezi wa Agosti

2022. Matokeo ya utafiti huo yanatarajiwa kutoa mapendekezo ya hatua za uimarishaji wa utumishi wa umma hapa Zanzibar na mwelekeo wa mageuzi ya utumishi yanayohitajika katika kuendeleza utumishi wa umma kwa kuzingatia hali ya sasa.

***Programu ya Uratibu wa ARKSUUB - Pemba***

47. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2022, programu ya Uratibu wa ARKSUUB imeratibu na kusimamia shughuli za utawala, utumishi na mipango ya Ofisi kwa upande wa Pemba kwa kusimamia mafunzo ya Maofisa Wadhamini, zoezi la uhakiki wa watumishi na tathmini ya raslimaliwatu kwa Wizara na Taasisi za Serikali wenye lengo la kubaini mahitaji na upungufu wa watumishi katika Wizara na Taasisi na kutoa miongozo mbali mbali ya kiutumishi. Aidha, Afisi imefuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi za Wizara ziliopo Pemba na kuhimiza uwajibikaji wa watumishi katika utoaji huduma bora kwa wananchi.

48. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **818,860,000**. Hadi kufikia Machi **2022,** Shilingi **294,619,140** zimepatikana sawa na asilimia 36.

## TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU.

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2021/2022 Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imesimamia ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo ya Chuo cha Utawala wa Umma, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Skuli ya Sheria kwa ajili ya utekelezaji wa program ziliomo katika taasisi hizo. Hatua za utekelezaji wa kazi katika taasisi hizo na fedha zilizopatikana ni kama ifuatavyo:

### *Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana*

50. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki jumla ya tirka 1,704 zimefunguliwa na tirka 879 zenye thamani ya shilingi **53,172,213,280** zimefungwa na warithi kupatiwa haki zao. Aidha, muda wa majaribio wa Mfumo wa uendeshaji wa mirathi kwa njia ya kieletroniki umemalizika na kutarajiwa kuanza kazi rasmi mwezi Julai 2022. Vile vile, mali zenye thamani ya Shilingi **611,399,701.95** kutokana na kodi ya nyumba 412 na mashamba 14 imekusanywa na kugawiwa kwa wanufaika.

51. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni imekusanya na kugawa Zaka na misaada ya kheri ya chakula, fedha, nguo na misahafu kwa wananchi wa Unguja na Pemba yenye thamani ya Shilingi **514,906,000**.

Kwa upande wa ushughulikiaji wa kesi na mizozo, Kamisheni imetoa ushauri wa kisheria kwa mashauri 86, imeshughulikia mizozo 92, kati ya hiyo 47 imepatiwa ufumbuzi, 36 inaendelea na tisa (9) imepelekwa Mahkamani. Jumla ya kesi 79 zimefuatiliwa katika Mahkama mbali mbali.

52. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Wakfu na mali ya Amana ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **1,267,200,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi **2022,** jumla ya Shilingi **593,445,830** sawa na asilimia 46.8 zimepatikana. Kati ya hizo, Shilingi **470,569,610** ni mishahara na Shilingi **122,876,220** ni matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi **132,930,533.20** zimekusanywa sawa na asilimia 67 kutokana na ada ya mirathi na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. ***(angalia kiambatanisho 1c)***

### *Chuo cha Utawala wa Umma*

53. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi **2022**, Chuo cha utawala wa Umma kupitia programu ya mafunzo ya muda mrefu kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 1,566 katika ngazi mbali mbali. Kati ya hao, 558 ni Watumishi wa Umma na 1,008 ni Wananchi wengine. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa Wakuu wa Taasisi zinazojitegemea 58 Unguja, kuhusu Maslahi ya Taifa, Uzalendo na umuhimu wake kwa Taifa na

Viashiria vikuu vya kupima ufanisi wa matokeo ya utekelezaji katika Taasisi za Umma.

Vile vile Chuo kimeandaa na kutoa mafunzo mafupi ya kuimarisha utendaji kazi kwa watumishi 61 waliokuwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**54. Mheshimiwa Spika,** watumishi 17 wa Chuo cha Utawala wa Umma wamejengewa uwezo juu ya Upimaji na Tathmini ya kazi na watumishi 42 wamepatiwa fursa ya kujiendeleza kitaaluma katika ngazi ya uzamili na uzamivu, kati ya hao, 24 ngazi ya uzamivu,15 ngazi ya uzamili na watatu (3) ngazi ya shahada ya kwanza. Mafunzo hayo yametolewa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma.

**55. Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa kutumia ruzuku ya Shilingi **1,503,500,000,** Hadi kufikia Machi 2022, Shilingi **1,109,260,265** zimepatikana sawa na asilimia **73.7.** Aidha, Chuo kimekadiria kukusanya Shilingi **2,024,415,000** kutokana na malipo ya ada za wanafunzi na kukusanya Shilingi **1,137,136,400** sawa na asilimia **56**.1. ***(angalia kiambatanisho 1c***)

### *Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma*

**56. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi **2022,** Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kupitia programu ya

kusimamia maadili ya viongozi wa umma imepokea na kuhifadhi Fomu za Tamko la Mali na Madeni kwa viongozi 2,473 waliowasilisha kwa wakati fomu zao katika Ofisi za Tume sawa na asilimia 99. Orodha kamili ya majina ya Viongozi wote waliowasilisha Fomu hizo kwa mwaka 2021/202, tayari imechapishwa katika Gazeti rasmi la Serikali kupitia toleo nambari 39 la mwaka 2022, la tarehe 28 Januari 2022, na taratibu za kisheria zinaendelea kuchukuliwa kwa Viongozi 11 waliochelewa kuwasilisha fomu zao za Tamko la Raslimali na Madeni katika Ofisi za Tume ya Maadili.

Katika kipindi hicho, Tume imefanya uhakiki wa taarifa za mali na madeni kwa viongozi wa umma 224 sawa na asilimia 112 ya shabaha iliopangwa kwa kipindi hicho.

Aidha, jumla ya malalamiko 18 ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi kuhusu matumizi mabaya ya madaraka, udhalilishaji wa kijinsia na utelekezaji wa familia yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya hayo, malalamiko matatu (3) uchunguzi wake umekamilika na kuwasilishwa kwenye vikao vya Tume kwa kusikilizwa na kutolewa uamuzi wa kufaa na malalamiko 15 yanaendelea na uchunguzi.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** tarehe 13/12/2021 Tume ya Maadili ya Viongozi kwa kushirikiana na taasisi za utawala bora imeadhimisha siku ya

Maadili na Haki za Binaadamu yenye kauli mbiu ya ''Piga vita Rushwa, Heshimu Haki za Binaadamu, Uadilifu na Uwajibikaji kwa Maendeleo ya Uchumi Endelevu". Vile vile, Tume imeandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Tume kwa Mwaka 2020/2021 na kuwasilisha kwa wakati katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi tarehe 15 Disemba 2021.

Kwa upande wa uelimishaji jamii kuhusu umuhimu wa kutunza maadili kwa viongozi wa umma, jumla ya mikutano 36 ya utoaji elimu kwa viongozi wa Wizara na Taasisi zake, Madiwani na Masheha wa Wilaya zote Unguja na Pemba imefanyika. Jumla ya vipindi sita (6) vya elimu kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na umuhimu wa kuimarisha maadili vimeandaliwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) na vipeperushi 3,520 vimetolewa kwa wananchi.

58. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **1,151,300,000**. Hadi kufikia Machi **2022**, Shilingi **431,932,225** zimepatikana sawa na asilimia **37.5** kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

### *Skuli ya Sheria Zanzibar*

59. **Mheshimiwa Spika,** Skuli ya Sheria Zanzibar imeanzishwa kwa Sheria Namb 13 ya mwaka 2019, na kuanza kazi zake rasmi tarehe 25 Mei

2021, baada ya uteuzi wa Viongozi wa Skuli hiyo. Mara baada ya kuanzishwa kwa Skuli hiyo na kupitia programu ya utoaji wa mafunzo ya vitendo kwa Wanasheria, kazi za uendeshaji wa mafunzo ya Sheria kwa Wanasheria zimeanza kutolewa katika Chuo cha Utawala wa Umma tarehe 17/01/2022, kwa kutumia Mtaala wa Skuli ya Sheria wa Tanzania Bara.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** Skuli imeanzisha udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Skuli hiyo kwa njia ya mitandao (online admission system) utakaowezesha kutambua uhalali wa vyeti vya wanafunzi hao na jumla ya wanafunzi 91 waliomba kujiunga na Skuli ya Sheria ambapo 59 walichaguliwa kujiunga na Skuli na 21 kati ya hao, wamesajiliwa na kuendelea na masomo sawa na asilimia 35.59. Aidha, Skuli imeendesha mafunzo elekezi ya wiki mbili kwa Majaji, Mahakimu wapya na Wanasheria 15 pamoja na Wakufunzi 27 kuanzia tarehe 14 hadi 25 Februari 2022.

Vile vile, Skuli imekamilisha Muundo wa Skuli ya Sheria na kuridhiwa na Baraza la Skuli na kuwasilishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa hatua za uidhinishwaji. Pia, Skuli imetayarisha Kanuni za nidhamu kwa wanafunzi na kanuni za mtihani na kuendelea na matayarisho ya Mpango Mkakati wa Skuli ya Sheria na Mitaala ya Skuli hiyo.

61. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **494,000,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi **2022**, Shilingi **183,725,376** zimepatikana sawa na asilimia **37.2.** Aidha, Skuli imekusanya mapato ya Shilingi **31,765,000** kutokana na malipo ya ada za wanafunzi na mafunzo mafupi ya kujenga uwezo. ***(angalia kiambatanisho 1c)***

## G02: MAHKAMA KUU

### *Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki*

62. **Mheshimiwa Spika,** programu ya usimamizi na upatikanaji wa haki inasimamia utoaji wa haki kupitia ngazi zote za mahkama kwa kutafsiri Sheria, kupokea, kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri yote ya jinai na madai yanayowasilishwa Mahakamani.

Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Mahkama imepokea na kusajili kesi 7,304 za jinai na madai zilizofunguliwa katika Mahkama mbali mbali na kuzitolea uamuzi. Kati ya hizo, kesi za jinai ni 5,498 na zilizotolewa uamuzi ni kesi 3,482 sawa na asilimia 63 na kesi 2,016 zinaendelea kusikilizwa.

Kwa upande wa kesi za madai, jumla ya kesi 1,816 zilifunguliwa na kesi 379 zimetolewa uamuzi sawa na asilimia 21 na zinazoendelea

Mahkamani ni kesi 1,427. Kesi zote hizo za jinai na madai zinajumuisha rufaa na maombi.

63. **Mheshimiwa Spika,** Mahkama maalumu ya kesi za udhalilishaji imepokea na kusajili kesi 383 na kuzitolea uamuzi kesi 83 sawa na asilimia 22 na kesi 300 zinaendelea Mahkamani. Aidha, Mahkama ya Kadhi imepokea na kusikiliza kesi 1,200 zilizofunguliwa katika Mahkama hiyo. Kati ya hizo, kesi 399 sawa na asilimia 33 zimetolewa uamuzi na kesi 801 zinaendelea. ***(angalia kiambatanisho nam 3)***

64. **Mheshimiwa Spika,** mashirikiano na wahusika wa Haki Jinai yameendelea kwa lengo la kuhakikisha kwamba mashauri yote yaliopo Mahkamani yanasikilizwa kwa haraka, uweledi na kutolewa uamuzi. Katika hili, vikao vitatu (3) vya wahusika wa Haki Jinai vimefanyika kujadili masuala mbali mbali ya jinai na changamoto zinazopunguza kasi ya usikilizaji wa mashauri na kupelekea hatua za kuzipatia ufumbuzi wa kufaa pamoja na kuadhimisha siku ya Sheria Zanzibar ambayo ilihusisha washiriki mbali mbali kutoka taasisi za Sheria na wananchi.

Aidha, jitihada maalum za kuharakisha usikilizaji wa kesi zimeendelea kuchukuliwa kupitia Mfumo wa Kuendesha kesi kwa njia ya kieletroniki (Case Management System) ambapo Mahkama ilipanga kuanza kutumia rasmi mfumo huo mwezi Februari 2022, baada ya kufanyiwa

majaribio na kuwapatia mafunzo watumiaji wa mfumo huo kwa awamu ya kwanza. Hata hivyo, kutokana na changamoto za kimtandao katika majengo ya Mahkama ya Vuga na Tunguu zoezi hilo halikuweza kufanyika. Matayarisho ya mfumo huo kwa upande wa Mahkama kuu Pemba yamekamilika.

65. **Mheshimiwa Spika,** Kamati maalum za nidhamu na maadili zimeundwa na kuanza kazi kwa ajili ya kuhakikisha uzingatiaji wa maadili katika utendaji wa Mahakama. Kamati zenyewe ni Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahakama ilioanzishwa chini ya Sheria Namb. 11/2018 Kifungu cha 35 na Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Mawakili na Vakili ilioundwa chini ya Sheria 1/2020 Kifungu cha 41.

66. **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa jengo la Mahkama Kuu Tunguu umekamilika na kukabidhiwa rasmi ambapo ufunguzi wa jengo hilo umefanyika tarehe 09/01/2022, na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Shughuli za kimahkama katika jengo hili zilianza rasmi tarehe 24/01/2022.

67. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilipangiwa jumla ya shilingi **8,246,000,000**. Hadi kufikia Machi **2022,** Shilingi **5,329,299,805** zimepatikana sawa na asilimia **64.62** kwa matumizi ya mishahara na matumizi

mengineyo. Mahkama ya Kadhi ilipangiwa shilingi **1,237,100,000** na imepokea ruzuku ya Shilingi **763,794,885** sawa na asilimia **61.74** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Aidha, jumla ya Shilingi **576,942,104** zimekusanywa na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 64.2. ***(angalia kiambatanisho 1c)***

## G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU

### *Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa huduma za Sheria*

**68.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, Mwanasheria Mkuu ndio Mshauri Mkuu wa Serikali kwa mambo yote ya kisheria. Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu Namba 6 ya 2013, imefananua kazi mbali mbali ambazo Afisi inafanya ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa taasisi mbali mbali za Serikali, Uandishi wa Miswada ya Sheria, Kanuni na kuandaa matangazo ya kisheria. Majukumu mengine yanayotekelezwa na Afisi hii ni kusimamia Kesi na Mashauri ya Madai kwa niaba ya Serikali, kuandaa Hati na Nyaraka za kisheria, kusimamia Mikataba yote ambayo Serikali ni sehemu ya Mikataba hiyo na kufanya mambo mengine ya kisheria yatakayowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu.

69. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 kupitia programu hii, jumla ya Miswada saba (7) ya Sheria iliandaliwa na Kanuni 15 za Sheria tofauti kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa Sheria hizo na ufanisi. Afisi imeandaa Matangazo ya Kisheria 134 kuhusu mambo mbali mbali na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. ***(angalia kiambatanisho nam 4)***

70. **Mheshimiwa Spika,** rasimu za Mikataba 538 zimefanyiwa mapitio na kutolewa ushauri, kati ya mikataba hiyo 130 ni ya ununuzi wa Bidhaa na Huduma, 74 Ujenzi, 62 Ushauri elekezi na 62 ni mikataba ya kodi. Aidha, Hati za Maelewano (MoU) 80 kuhusu masuala ya elimu, afya, ufugaji, nishati, utawala bora, maji na kilimo zimefanyiwa mapitio na kutolewa ushauri katika taasisi husika.

Kwa kipindi hiki kuna ongezeko la mapitio ya rasimu za mikataba la zaidi ya asimilia Mia Moja ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2020/2021. Hali hii inadhihirisha wazi nia ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar kwa kuanzisha miradi mbali mbali itakayowanufaisha.

Kwa upande wa kesi za madai, Afisi iliendelea kuiwakilisha Serikali kwenye mashauri ya kesi

za madai 233 katika Mahkama mbali mbali na kufuatilia Indhari za kuishtaki Serikali 42 zilizowasilishwa. Kati ya hizo, kesi 20 zimemaliza na kutolewa hukumu na kesi 32 mpya zimefunguliwa. Katika kipindi hiki jumla ya kesi 66 zinaendelea kusimamiwa katika Mahkama za Unguja na kesi sita (6) zinasimamiwa kwa upande wa Pemba.

71. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilipangiwa jumla ya shilingi **2,398,700,000**. Hadi kufikia Machi **2022,** Shilingi **1,420,317,730** zimepatikana sawa na asilimia 59.21 kwa ajili ya matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

## G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

### *Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai*

72. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeendesha jumla ya kesi za jinai 889 katika Mahkama mbali mbali za Unguja na Pemba. Kati ya kesi hizo 269 ni kesi za udhalilishaji, 144 ni kesi za madawa ya kulevya na kesi 476 zinahusiana na makosa mengineyo. Afisi pia imepokea majalada 389 kutoka Jeshi la Polisi na kuyatolea maoni kisheria.

Katika kipindi hiki, Afisi imeshughulikia majalada ya kesi za udhalilishaji na kutolewa

uamuzi wa mashtaka ndani ya siku moja na zisizozidi siku tatu ili kuharakisha uendeshaji wa kesi. Aidha, Afisi imeshirikiana na wahusika wa haki za jinai kama vile Mahkama, Chuo cha Mafunzo, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na Chama cha Wanasheria Zanzibar ili kuhakikisha usimamizi bora wa haki za jinai kwa wananchi na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazojitokeza katika uendeshaji wa kesi za udhalilishaji.

73. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya Mashahidi 2,821 walipokelewa na kutoa ushahidi katika kesi za jinai baada ya kupatiwa ushauri wa kisheria unaostahiki ili kurahisisha uendeshaji wa kesi. Idadi ya Mashahidi imeongezeka kutokana na muamko wa wananchi katika kutoa ushahidi na kufuatilia mwenendo wa kesi za udhalilishaji. Afisi imefanikiwa kuanzisha kitengo cha kusimamia Haki za Binaadamu, Waathiriki na Mashahidi wa kesi za jinai katika kuhakikisha waathirika na mashahidi wanapata taarifa za mwenendo wa kesi zao ili kurahisisha uendeshaji wa kesi.

Kwa upande wa mafunzo ya watumishi, Waendesha Mashtaka 81 wamepatiwa mafunzo ya uendeshaji wa kesi za udhalilishaji na watoto, ulinzi wa waathirika na mashahidi, maadili na maeneneo ya fedha na ununuzi.

Vile vile, Afisi imeendelea kutoa mafunzo ya sheria ya muda mfupi na muda mrefu

kupitia Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar, katika ngazi ya cheti na stashahada na kuongeza idadi ya wanafunzi kufikia 90. Kati ya hao, wanafunzi 43 ni wa ngazi ya cheti na 47 ni wa ngazi ya Stashahada.

74. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilipangiwa jumla ya shilingi **3,183,693,315**. Hadi kufikia Machi 2022, Shilingi **1,829,406,218** zimepatikana sawa na asilimia 57.46. Kati ya hizo, Shilingi **1,362,534,218** kwa ajili ya mishahara na Shilingi **403,692,000** kwa matumizi mengineyo na shilingi **63,180,000** zimepatikana kwa ajili ya ruzuku ya Chuo sawa na asilimia 31.9.

## G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

### *Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria*

75. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2022, Tume ya Kurekebisha Sheria kupitia programu hii imefanya mapitio ya Sheria 17 zilizokamilika kama ifuatavyo: - Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya Mwaka 2011; Sheria ya uanzishwaji wa Taasisi ya Wahasibu Wakaguzi wa Hesabu na Washauri wa Kodi; Sheria ya usimamizi wa Sekta ndogo za Fedha (Microfinance); Sheria ya Madawa ya Kulevya; Sheria ya Mufti; Sheria ya Kuanzishwa kwa Jumuiya; Sheria ya Mfuko

wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) hasa katika eneo la kikokotoo cha Mafao ya Wastaafu; Sheria ya Ardhi Eneo la Migogoro ya Ardhi na Utatuzi wake; Sheria ya Kuanzishwa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Sheria ya Serikali Mtandao (e – Government); Sheria ya Leseni za Biashara; Sheria ya Mazingira; Sheria ya Rushwa na Uhujumu Uchumi; Sheria ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari; Sheria ya Kuzuiya Utakatishaji wa Fedha Haramu Nam. 1 ya mwaka 2009; Sheria ya Kilimo eneo linalohusu masuala ya Mbegu; na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Nam. 15 ya mwaka 1986.

76. **Mheshimiwa Spika,** Tume inaendelea na hatua ya ukusanyaji wa maoni na uandishi wa ripoti wa Sheria 11 zilizofanyiwa mapitio kwa ajili ya kuwasilishwa Serikalini kwa hatua zaidi. Sheria zenyewe ni: Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982; Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015; Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Nam. 4 ya mwaka 2012; Sheria ya Mafuta na Gesi Nam. 6 ya mwaka 2016; Sheria ya Wakala wa Bohari; Sheria ya Uhifadhi wa Mimea Nam. 9 ya mwaka 1997; Njia Mbadala wa Utatuzi wa Migogoro; Sheria ya Utalii; Sheria ya Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) Nam.4 ya mwaka 2013; Eneo la Uchumi wa Buluu; na Sheria ya Njia Mbadala ya Utatuzi wa Migogoro (Aleternative Disputes Resolution)

77. **Mheshimiwa Spika,** Tume imewapatia mafunzo ya muda mrefu watendaji wanne (4) katika fani za Sheria, Raslimaliwatu, Jinsia na Uchumi na mafunzo mafupi ya utafiti wa Sheria kwa ajili ya kuongeza ujuzi wa watumishi hao na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Pia, Tume imetoa elimu kwa Umma kupitia Vyombo vya habari mbali mbali ikiwemo redio, TV na mitandao ya kijamii na mikutano kuhusu majukumu ya kazi zake na umuhimu wa Mapitio ya Sheria.

78. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **1,739,000,000**. Hadi kufikia Machi 2022, Shilingi **629,197,835** zimepatikana sawa na asilimia 36. Kati ya hizo Shilingi **386,197,835** kwa ajili ya mishahara na Shilingi **243,000,000** kwa matumizi mengineyo.

## E04: OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

### *Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa fedha na Rasilimali za Umma*

79. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imefanya ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Wizara, Idara na Taasisi za Umma za mwaka 2020/2021 kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na kuwepo kwa matumizi bora ya rasilimali za Umma pamoja

na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za Umma. Katika kipindi hiki, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ipo katika hatua za mwisho kukamilika ili iweze kuwasilishwa katika mamlaka husika kabla ya kuwasilishwa katika mkutano wa Baraza la Wawakilishi.

80. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanya ukaguzi wa pamoja wa fedha za UVIKO 19 na miradi ya TASAF, MKURABITA ruzuku za Vyama vya Siasa, michango ya Mwenge wa Uhuru, mikato ya fedha za wafanyakazi wa Taasisi za Muungano na ukaguzi wa gawio la Benki Kuu (BOT).

Aidha, Ofisi imewapatia mafunzo mbali mbali ya uhasibu na ukaguzi wa viwango vya juu kitaifa na kimataifa, mafunzo ya viwango vya ukaguzi wa Mashirika ya Umma na mafunzo ya ukaguzi jumuishi watendaji wa Ofisi ya CAG 53 kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji ili kuwa na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

81. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **4,382,200,000**. Hadi kufikia Machi 2022, Shilingi **2,600,487,165** zimepatikana sawa na asilimia 59.34. Kati ya hizo shilingi **1,764,831,415** zimetumika kwa mishahara na shilingi **835,655,750** kwa ajili ya matumizi mengineyo. ***(angalia kiambatanisho nambari 1c)***

## EO5: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI

***Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.***

82. **Mheshimiwa Spika,** jitihada mbali mbali za kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi zilichukuliwa kwa kushirikiana na taasisi za haki jinai ili kupunguza vitendo vya rushwa hapa nchini kwa kuzingatia Sheria Namb.1 ya mwaka 2012, Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar.

Hadi kufikia Machi 2022, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi imepokea na kushughulikia tuhuma 83 zinazohusiana na kushawishi, kuomba na kupokea rushwa, ubadhirifu wa mali na mapato, matumizi mabaya ya Ofisi, magendo, matumizi mabaya ya mali na kukwepa kulipa kodi. Kati ya hizo, tuhuma 70 zinaendelea na uchunguzi, saba (7) zimewasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, kesi moja inaendelea kusikilizwa Mahkamani na kesi mbili (2) zimetolewa uamuzi. ***(angalia kiambatanisho nam 5)***

Katika kipindi hiki, jitihada za uokoaji na urejeshaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa na uhujumu wa uchumi ziliendelea. Mamlaka imeokoa na kurejesha kiasi cha Shilingi 54,445,000 kupitia makosa ya

magendo, matumizi mabaya ya mali na mapato na matumizi mabaya ya ofisi.

83. **Mheshimiwa Spika,** kazi za mapitio ya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Namba 1 ya mwaka 2012, zimefanyika kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria na kuainisha mapungufu ya kisera na kisheria yaliomo katika Sheria hiyo ambayo tayari yanashughulikiwa na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kama msimamizi wa Sera ili yaweze kuwasilishwa Serikalini kwa hatua zaidi. Tume imependekeza kufutwa kwa Sheria hiyo na kutunga Sheria mpya ili iendane na hali ya sasa ya kiuchumi na kijamii pamoja na dhamira ya Serikali ya kudhibiti rushwa na uhujumu wa uchumi.

Vile vile, Mamlaka imeendelea kuelimisha jamii kuhusu athari na madhara ya rushwa na uhujumu uchumi kwa kutoa elimu katika Taasisi 23 za Serikali na zisizo za kiserikali, Maofisa wa kikosi cha Zimamoto, Wakufunzi, watendaji na wanaharakati wa mapambano ya udhalilishaji wa kijinsia.

84. **Mheshimiwa Spika,** juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kukabiliana na vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi hapa Zanzibar zimeleta mafanikio makubwa ya kuongeza nidhamu, uadilifu na uwajibikaji katika utumishi wa umma, biashara,

uwekezaji, ukusanyaji mapato na matumizi ya madaraka na fedha za umma. Mafanikio haya yameijengea Serikali uwezo imara wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma bora kwa wananchi.

85. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **2,159,100,000**. Hadi kufikia Machi **2022**, Shilingi **1,311,138,312** zimepatikana sawa na asilimia 60.72 kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

## E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

***Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma***

86. **Mheshimiwa Spika,** kazi za usimamizi wa utumishi wa umma zimeendelea kutekelezwa kupitia programu hii ili kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma yanasimamiwa na kuendeshwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali kama inavyotolewa na Ofisi kuu ya Utumishi wa umma.

Katika kipindi hiki Kamisheni imepokea na kuridhia miundo ya Taasisi za Umma 38. Aidha, Kamisheni imekusanya taarifa za kiutumishi kutoka Wizara na taasisi 106 pamoja na mashirika manane (8) kwa ajili ya kuangalia uzingatiwaji wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma katika utoaji wa huduma.

Aidha, Kamisheni ilipokea na kushughulikia Rufaa tisa (9) za kiutumishi kuhusu madai ya kufukuzwa kazi na madai ya maslahi mbali mbali kutoka kwa watumishi wa umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka zao za Nidhamu katika Utumishi wa Umma na kutoa uamuzi wa kufaa.

Kwa upande wa mafunzo, watumishi wawili (2) wamelipiwa ada za mafunzo ya Shahada ya kwanza katika fani ya ukatibu muhtasi na Raslimaliwatu na kuwapatia mafunzo elekezi ya muda mfupi kwa waajiriwa wapya wanane (8).

87. **Mheshimiwa Spika,,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **1,364,300,000** na hadi kufikia Machi 2022, Shilingi **636,210,016** zimepatikana sawa na asilimia 46.63 kwa malipo ya mishahara na matumizi mengineyo.

## E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

### *Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini*

88. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utumishi Serikalini imeidhinisha ajira ya kudumu kwa watumishi 22, ajira ya mkataba kwa watumishi 269, kuthibitisha kazi watumishi 1,878, kupandisha daraja watumishi 636 na kubadilisha kada watumishi 140 na kuidhinisha nyongeza ya muda wa utumishi kwa watumishi 3. Aidha,

Tume imeidhinisha kustaafu kwa lazima watumishi 512, kustaafu kwa hiyari watumishi 18, kustaafu kwa maradhi watumishi wanane 16 na kuridhia kuacha kazi watumishi watano (9) kwa mujibu wa Kanuni ya 25 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014. **(angalia kiambatisho namb. 6a&b)**

Katika kipindi hicho, Tume imepokea, kusikiliza na kuyatolea uamuzi malalamiko sita (9), kuidhinisha kufukuzwa kazi watumishi 30 na kuwaachisha kazi watumishi tisa (9).

89. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **648,600,000**. Hadi kufikia Machi **2022**, Shilingi **314,473,440** zimepatikana sawa na asilimia 48.48 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo.

## C. MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

90. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa kutumia fursa hii kutoa maelezo ya muelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha **2022/2023** kwa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

91. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutumia jumla ya Shilingi **49,662,665,000**. Kati ya hizo, Shilingi **22,608,249,000** zimepangwa

kutumika kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na shilingi **23,793,011,000** zimepangwa kutumika kwa matumizi mengineyo.

Aidha, Shilingi **3,261,405,000** zimepangwa kutumika kwa utekelezaji wa program ya miradi ya maendeleo ikijumuisha mchango wa Shilingi **1,581,000,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo **(angalia kiambatanisho namb 2).**

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi imepanga kutumia ruzuku ya Shilingi **2,072,600,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Chuo cha Utawala wa Umma na Skuli ya Sheria na kukusanya jumla ya Shilingi **1,707,000,000** kupitia vyanzo vya mapato vya Ofisi kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali **(angalia kiambatanisho nam 2 &3).**

## D. VIPAUMBELE VYA OFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**93.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023** Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kutekeleza Mpango wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria wa Awamu ya Pili;

ii. Kutayarisha na kutoa miongozo ya Utoaji wa Msaada wa Kisheria na kuandaa Mpango kazi wa Kitaifa (NPA);

iii. Kuendelea na Utekelezaji wa Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma kwa Awamu ya Pili;

iv. Kuendelea kuimarisha utendaji katika taasisi za Sheria na kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali;

v. Kuendelea na kazi za uimarishaji wa miundombinu ya majengo ya Mahkama kwa kufanya matengenezo ya majengo ya mahkama yaliopo na kuanzisha miradi ya ujenzi wa majengo mapya ya mahkama; na

vi. Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma na masuala ya utawala bora;

***Malengo Makuu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023***

**94.** **Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria;

ii. Kusikiliza kesi na kutoa maamuzi ya haraka na kwa wakati;

iii. Kuhakikisha Upatikanaji wa Msaada wa Kisheria katika maeneo yote ya kijamii;

iv. Kuanzisha Jukwaa la sekta ya Sheria na kusimamia masuala ya Dini;

v. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Raslimaliwatu wa mwaka 2022/2023.

vi. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa mafunzo ya watumishi wa umma kwa ajili ya upatikanaji wa Rasilimali Watu wenye sifa;

vii. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika shughuli na utoaji wa huduma za Serikali; na

viii. Kuimarisha misingi ya utawala bora na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali.

**95.** **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha maelezo ya programu za Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:-

**96.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepata mafungu manne mapya ya bajeti yaliotolewa kwa taasisi za Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar (G11), Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana (G12), Wakala wa Serikali Mtandao (G13) na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma (G15). Mafungu hayo yamepelekea Ofisi kuwa na jumla ya mafungu ya bajeti 13 yaliopangwa kutekelezwa kupitia Programu kuu 15 kama ifuatavyo: i) Programu ya Usimamizi wa masuala ya Sheria;

ii) Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora; iii) Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma; iv) Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa ARKSUUB; ziliomo katika fungu **G01**; na v) Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki **G02**; vi) Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria **G03**; vii) Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai **G04**, viii) Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria **G05;** ix) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini **G11**, **G12**; x) Programu ya Huduma za Serikali Mtandao **G13**; xi) Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma **G15**; xii) Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma **E04**; xiii) Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi **E05**; xiv) Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma **E07**; xv) Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini **E08**.

97. **Mheshimiwa Spika,** kati ya programu hizi, programu kuu nne (4) za fungu **G01** zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu na Programu kuu 11 zinatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea.

## G01: AFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

### *Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria.*

98. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu ya Usimamizi wa Msaada wa Kisheria itaendelea na utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria katika maeneo yote ya utoaji wa haki. Idara itaandaa Mpango wa Kitaifa wa Msaada wa Kisheria (NPA), mikutano na wahusika wa mapambano ya masuala ya udhalilishaji, vikao vya robo mwaka vya wahusika wa msaada wa kisheria na kutoa mafunzo ya ushauri nasihi kwa waathirika wa vitendo vya udhalilishaji.

Idara pia, itachapisha Jarida la Msaada wa Kisheria, kuadhimisha wiki ya msaada wa kisheria, kukamilisha ripoti ya mwaka ya msaada wa kisheria na kuendeleza vituo vya msaada wa kisheria katika Vyuo Vikuu.

Aidha, Idara itawajengea uwezo watendaji wake kwa kuwapatia mafunzo mafupi na muda mrefu na kujenga mahusiano na mashirikano kwa taasisi za msaada wa kisheria.

99. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi

**283,240,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

***Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora.***

100. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, programu ya usimamizi wa Utawala Bora imepanga kukamilisha Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2022, na kuanzisha taratibu za utungaji wa Sheria ya Usimamizi wa Utawala Bora ya mwaka 2023. Idara itaijengea uwezo jamii kuhusu masuala ya utawala bora kwa kutoa elimu ya Utawala Bora kupitia mikutano na maonyesho ya kitaifa, vyombo vya habari na kutayarisha Jarida la Utawala Bora linalototolewa kila mwaka.

Aidha, Idara itaandaa Kongamano la Utawala Bora na kuadhimisha siku ya Maadili na Haki za Binaadamu kwa kushirikiana na taasisi za Utawala Bora na Kufanya tathmini ya Utawala Bora.

101. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **306,353,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

***Programu ya Uendelezaji wa Watumishi wa Umma.***

102. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma inahusisha programu ya Mipango na Maendeleo ya Watumishi na programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi zinazotekelezwa kupitia Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.

Kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, Idara ya Mipango Rasilimali Watu kupitia programu ndogo ya Mipango na Maendeleo ya Watumishi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Rasilimali Watu wa mwaka 2023/2024, katika Utumishi wa Umma, kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Taasisi za Umma na upatikanaji wa mafunzo yanayotolewa na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kuongeza fursa za mafunzo kwa watumishi wanaohitaji kujiendeleza.

Aidha, Idara kupitia programu hii, itaendelea kuratibu mafunzo ya Wastaafu, kukamilisha Sera ya Mafunzo ya Watumishi wa Umma na kuwapatia mafunzo ya matumizi ya Mfumo jumuishi wa taarifa za Raslimaliwatu na Mshahara watumiaji wa mfumo huo kutoka katika taasisi mbali mbali za umma.

103. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **472,210,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

104. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi inayotekelezwa na Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi itafanya mapitio ya Miundo ya Taasisi za Serikali kwa kuzingatia Hati Idhini ya Serikali ilizotolewa, kutoa mafunzo ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, kuandaa Mkataba wa Utendaji kazi kwa Viongozi na kutoa miongozo. Aidha, Idara itaaandaa na kufanya mapitio ya Matoleo na Miongozo ya Kiutumishi na kufuatilia utekelezaji wa Mkataba wa utoaji wa Huduma kwa Mtaka Huduma, zoezi la upimaji utendaji kazi pamoja na Muundo wa Utumishi kwa Wizara, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea.

105. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** jumla ya Shilingi **543,000,000.00** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

### *Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ARKSUUB*

106. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo tatu (3) zinazotekelezwa kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, na Afisi Kuu- Pemba.

Kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** programu ya Uendeshaji na Utawala wa Afisi inayotekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi itaendelea kusimamia nidhamu na kulipa stahiki za watumishi na kuhudumia uendeshaji wa Ofisi na kufanya matengenezo ya vifaa na miundombinu ya Ofisi.

Kupitia programu hii, Idara itafanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu wa Wizara wa miaka mitano, kufanya tathmini ya utendaji kazi, tathmini ya uwezo wa Watumishi (Capacity Needs Assessment) na tathmini ya Mkataba wa Utoaji Huduma kwa wananchi. Idara itasimamia Mfumo wa Taarifa za watumishi na mfumo wa usimamizi wa fedha na kuimarisha Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu na kuanzisha Mfumo wa Mawasiliano ya Ofisi kwa njia ya kieletroniki (e-office)

Vile vile, Idara itasimamia utekelezaji wa Mpango wa ununuzi na kufanya vikao vya Bodi ya zabuni; kutekeleza Mpango wa Ukaguzi wa Hesabu wa ndani na kufanya vikao vya Kamati ya Ukaguzi;

Pia, Idara itaendelea kuripoti matukio mbalimbali ya Wizara katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii na kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara.

107. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** jumla ya Shilingi **2,585,374,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

108. **Mheshimiwa Spika,** programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti itaendelea kuratibu mapitio na matayarisho ya Sera, Sheria, mipango na bajeti ya Afisi pamoja na kufuatilia utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Wizara na kufanya tathmini. Aidha, Idara itaratibu na kufanya tafiti za sekta ya Sheria ya utumishi na Utawala Bora na kuandaa nyaraka za kisera na kisheria zitakazowasilishwa Serikalini.

Vile vile, Idara itaratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria na Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma wa Awamu ya Pili unaoendelea. Kupitia programu hizi, Idara itaratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za program za miradi ya Kurahisisha Upatikanaji wa Huduma katika Utumishi wa Umma *(Public Service Acceleration Program);* Kujenga uwezo wa Viongozi wa Umma (*Transformative Leadership*);

Upatikanaji wa Haki za Wanawake na Wasichana katika eneo la kesi za Udhalilishaji (*Access to Justice for Women & Girls on GB cases)* na Uwezeshaji wa Kisheria na Upatikanaji wa Haki *(Legal Empowerment & Acees to Justice)* zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia ufadhili wa Washirika wa Maendeleo.

**109.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **363,010,000** zimepangwa kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2).**

**110.** **Mheshimiwa Spika,** programu ya Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Afisi Kuu Pemba itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli zote za utawala na utumishi, mipango na bajeti zinazotekelezwa na Afisi kwa upande wa Pemba.

**111.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **572,573,573** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**.

## TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU- G01

### *Chuo Cha Utawala wa Umma*

**112. Mheshimiwa Spika,** Chuo Cha Utawala wa Umma kupitia programu za mafunzo mafupi na muda mrefu kimepanga kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo wa watumishi wa umma na kutoa mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wanaongia katika ajira kwa mara ya kwanza ili kuondoa upungufu na mahitaji katika sekta za umma. Chuo kitafanya tafiti mbali mbali za kubaini upungufu na mahitaji yaliyopo katika sekta ya umma na kutoa huduma ya ushauri elekezi kwa taasisi hizo.

Aidha, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wa umma na wananchi katika ngazi ya Shahada, Stashahada na Astashahada kwa ajili ya kuiwezesha Serikali kujitegemea na kuwa na wataalamu wake.

**113. Mheshimiwa Spika,** ili kukiwezesha Chuo kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, kimepangiwa kutumia ruzuku ya shilingi **1,433,700,000** kati ya hizo shilingi **1,380,700,000** kwa ajili ya mishahara na **53,000,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Aidha, Chuo kimepanga kukusanya Shilingi **2,035,900,000** kutokana na malipo ya ada za wanafunzi **(angalia kiambatanisho nam 2)**

*Skuli ya Sheria Zanzibar*

**114. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Skuli ya Sheria Zanzibar kupitia programu ya mafunzo ya Sheria kwa vitendo imepanga kutoa mafunzo ya vitendo kwa Wahitimu wa Sheria katika ngazi ya Shahada ya kwanza, kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wanasheria wa Serikali na kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo Majaji, Mahakimu, Makadhi, Mawakili Wasaidizi wa Sheria na Watoa Msaada wa Sheria. Skuli itafanya utafiti wa masuala ya kisheria na kuandaa Mtaala wa Vakil watakaowakilisha Wadaawa katika Mahkama za Kadhi na Mahkama ya Mwanzo.

**115. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **529,500,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya ruzuku ya matumizi mengineyo. Aidha, Skuli ya Sheria imepanga kukusanya Shilingi **379,000,000** kupitia malipo ya ada za wanafunzi na uendeshaji wa mafunzo mafupi.

## G02: MAHKAMA KUU

*Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki*

**116. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka **2022/2023**, Mahkama itaendelea na utekelezaji wa jukumu la kupokea na kusikiliza mashauri na kutoa uamuzi kwa wakati, kuhakikisha mfumo wa

kisasa wa kuendesha kesi unaimarika na kufanya matengenezo ya majengo ya Mahkama ya Vuga Unguja, Mahkama ya Wete na Konde Pemba. Aidha, juhudi za kuanza ujenzi wa Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja zitaendelezwa baada ya kupatikana kwa eneo la ujenzi wa jengo hilo ambalo tayari limeshapimwa na hatua za kupatiwa hati miliki zinaendelea. Pia ujenzi wa majengo wa mahkama za mikoa ya kaskazini pemba na mjini magharibi unatarajiwa kuanza katika mwaka ujao wa fedha.

117. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **17,363,600,000** zimepangwa kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya hizo, Mahkama Kuu shilingi **16,096,800,000** na Mahkama ya Kadhi shilingi **1,266,800,000.** Aidha, Mahkama ya Kadhi imepangiwa kukusanya shilingi **1,278,069,860 (angalia kiambatanisho nam 2 & 3)**

## G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU

### *Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa huduma za Sheria*

118. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia programu hii itaendelea na kuiwakilisha Serikali Mahakamani dhidi ya kesi

zote za madai, kuandaa Miswada ya Sheria mbali mbali na kuiwasilisha Baraza la Wawakilishi na kuandaa Matangazo ya Kisheria na kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali. Afisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Serikali na kutoa ushauri wa kisheria katika Mikataba na Mashirikiano ya Kikanda na kimataifa. Aidha, Afisi itawapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watumishi wake kuhusu uendeshaji wa kesi kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kusimamia majukumu yao kwa ufanisi.

119. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **3,195,300,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

## G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

***Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai***

120. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itaendelea na kazi ya uendeshaji wa kesi za jinai katika Mahkama za Unguja na Pemba, kuratibu uendeshaji wa mashtaka ya mwanzo na taasisi zilizoidhinishwa, shughuli za upelelezi na kuanzisha mfumo wa kidigital katika utoaji wa

huduma za Mashtaka na kuwasaidia waathirika na mashahidi wa kesi za jinai.

Aidha, Afisi itawapatia mafunzo ya kujenga uwezo na kuongeza utaalamu wa Waendesha Mashtaka, ili waweze kutekeleza majukumu yao ya uendeshaji wa kesi mahkamani kwa ufanisi na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti.

121. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **3,509,430,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi **211,500,000** ni ruzuku kwa ajili ya Kituo cha Mafunzo ya Sheria**. (angalia kiambatanisho nam 2)**

## G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

### *Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria*

122. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023** Tume ya Kurekebisha Sheria kupitia programu hii imepanga kufanya mapitio ya Sheria mbali mbali na kuimarisha ufafiti wa kisheria. Katika kipindi hiki Tume itaendeleza na kuimarisha tovuti ya Tume na kuwapatia mafunzo ya utafiti wa Sheria watendaji wake ili kuwawezesha kutekeleza vyema kazi za utafiti

wa Sheria na majukumu yao ya kila siku. Vile vile, Tume itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya Tume kupitia vipindi vya redio na Televisheni, makongamano na semina.

123. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **1,901,790,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

## G14: OFISI YA MUFTI MKUU ZANZIBAR

### *Programu ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masula ya Kiislamu*

124. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mufti Mkuu kupitia Programu ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masula ya Kiislamu itaendelea itaendelea kutoa fatwa na kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi mzuri wa masuala ya Kiislamu; kutoa miongozo ya Kiislamu ya kusimamia Misikiti, Madrasa na Walimu wa Madrasa kwa mujibu wa Sheria ilioanzisha taasisi hiyo. Ofisi itaratibu na kusimamia uandaaji wa mihadhara, warsha, semina na mikutano ya Kiislamu, sherehe na maadhimisho ya Kiislamu na kutangaza kuandama kwa mwezi kwa mujibu wa Sheria pamoja na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya dini ya kiislamu kupitia

vyombo vya habari. Ofisi pia, itaratibu kazi za kitafiti za Kiislamu zinazoandaliwa na Taasisi za Serikali na binafsi na kuratibu na kusajili misikiti, madrasa, maahad, taasisi, makundi na jumuiya za Kiislamu.

125. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **1,208,100,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

## G12: KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

### Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Mirathi, Zakka na Misaada

126. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kupitia programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Mirathi, Zakka na Misaada imepanga kutoa huduma za Mirathi, Wakfu na Amana katika Wilaya zote za Unguja na Pemba na kukusanya Zaka na Misaada ya kheri. Vile vile, Kamisheni itaendelea na utoaji wa huduma za Hijja na kuanzisha Mfuko wa Hijja ili wananchi waweze kutekeleza wajibu wao.

127. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha

**2022/2023**, jumla ya Shilingi **1,309,750,000** zimepangwa kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)** Aidha, Kamisheni imekadiria kukusanya shilingi **220,000,000** kutokana na ada ya Mirathi.

## G13: WAKALA WA SERIKALI MTANDAO

### *Programu ya Huduma za Serikali Mtandao*

**128. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** kupitia programu hii, Wakala wa Serikali Mtandao itaendelea kuimarisha huduma za Serikali Mtandao katika uendeshaji wa shughuli za Serikali ili kuwa na muunganiko mzuri na wa kuaminika utakaowezesha utoaji wa huduma za kielektroniki katika utumishi wa umma.

Katika kipindi hiki, Wakala itaongeza uwezo wa Taasisi za Umma kutekeleza mipango ya Serikali Mtandao, upatikanaji wa huduma za kielektroniki na Rasilimali ya pamoja ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za Umma na kutoa miongozo mbali mbali ya usimamizi wa masuala ya TEHAMA.

**129. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **1,909,280,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

## G15*:* TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

### *Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi*

130. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kupitia programu hii kwa mwaka wa fedha **2022/2023** itaendelea kupokea, kuhifadhi na kuhakiki taarifa za mali na madeni ya viongozi wa Umma, kuelimisha viongozi wa umma na wananchi juu ya umuhimu wa kuzingatia maadili katika utekelezaji wa majukumu yao ya uongozi. Tume itapokea malalamiko ya uvunjwaji wa Sheria ya Maadili na kufanya uchunguzi, kusikiliza na kutoa uamuzi dhidi ya tuhuma za uvunjwaji wa maadili ya viongozi na kuadhimisha siku ya maadili duniani.

131. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **1,337,800,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida **(angalia kiambatanisho nam 2)**

## E04: AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

### *Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma*

132. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, itaendelea na ukaguzi wa hesabu za Wizara, Mashirika, Taasisi za Serikali na miradi ya maendeleo za mwaka 2021/2022 kwa kutumia viwango vya Ukaguzi vya kitaifa na kimtaifa pamoja na kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi.

133. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **4,801,100,000** zimepangwa kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

## E05: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

### *Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi*

134. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, itaendelea kufanya

uchunguzi wa tuhuma na makosa ya rushwa na uhujumu wa uchumi na kufuatilia matumizi ya fedha za Umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aidha, Mamlaka itakamilisha marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Namb.1 ya mwaka 2012 na kuandaa Taarifa ya Hali ya Rushwa ya Mwaka 2022 na kuiwasilisha katika Mamlaka husika.

Vile vile, Mamlaka itatoa elimu kwa umma kuhusu athari na madhara ya Rushwa na Uhujumu Uchumi na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watumishi wake.

135. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **4,544,600,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

## E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

### *Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma*

136. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka **2022/2023** Kamisheni itaendelea kufanya Uchambuzi wa Miundo ya Taasisi, Miundo ya Utumishi na Miundo ya Mishahara 24 itakayowasilishwa Kamisheni.

Katika kipindi hiki, Kamisheni itafanya mapitio, kuchapisha na kujenga uelewa wa Muongozo wa ukusanyaji taarifa katika Utumishi wa Umma na Muongozo wa uandaaji wa Miundo ya Utumishi, Taasisi na Mshahara ya taasisi za umma. Kamisheni pia, itajenga uwelewa wa Muongozo wa Usimamizi wa masuala ya Nidhamu katika Utumishi wa Umma kwa watumishi wa umma na viongozi.

Aidha, Kamisheni itafanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi za umma 32, ukaguzi maalumu katika taasisi nne (4) na ukaguzi wa kushtukiza katika taasisi za umma nne (4) Unguja na Pemba. Aidha, Kamisheni itapokea na kushughulikia rufaa 12 kutoka kwa watumishi na mamlaka za nidhamu, kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini katika Utumishi wa Umma na kuandaa Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2021.

137. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **1,447,300,00** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2)**

## E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

### *Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini*

138. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utumishi Serikalini kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, itaendelea kusimamia shughuli za ajira katika utumishi wa umma kwa kuzingatia vigezo na sifa zinazostahiki, kusimamia haki na nidhamu za watumishi kwa kupokea na kusikiliza malalamiko ya watumishi ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na mamlaka za nidhamu zilizo chini ya Tume na kukamilisha mfumo wa maombi ya ajira kwa njia ya kieletroniki.

Aidha, Tume itaratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba, nyongeza za muda wa utumishi, kuthibitisha kazi, kubadilisha kada, kupandisha daraja na kuidhinisha likizo bila ya malipo na kustaafu kwa watumishi wa Serikali.

139. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, jumla ya Shilingi **720,890,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2).**

## E. SHUKRANI

140. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 katika utekelezaji wa majukumu yetu. Shukurani za pekee ziwaendee Washirika wa Maendeleo walioendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza programu na mipango yetu ya uimarishaji sekta ya Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuleta maendeleo. Naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuawataja wachache ambao ni: Jamhuri ya Watu wa China, Korea ya Kusini, India, Saudi Arabia, Oman na Malaysia. Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (UNDP), Jumuiya ya Kimataifa ya Wanawake (UN Women), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Legal Service Facility (LSF), Benki ya Dunia (World Bank), Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IDB), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuzuia Uhalifu na Madawa ya Kulevya (UNODC) na Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma (AAPAM).

141. **Mheshimiwa Spika,** nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru viongozi wenzangu na nikianza na Nd. Seif Sh. Mwinyi, Katibu Mkuu, Nd. Mansura Mosi Kassim, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wote

wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Mrajis wa Mahakama Kuu, Manaibu Warajis, Mtendaji Mkuu wa Mahkama, Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wote, Mkurugenzi wa Mashtaka na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Mufti Mkuu na Kadhi Mkuu kwa kuendelea kusimamia utoaji wa haki kwa haraka na ufanisi wa hali ya juu.

Vile vile, nawashukuru, Wenyeviti wa Tume na Kamisheni, Makamishna na Wajumbe wote waliomo katika taasisi hizi, Wakuu wa Vitengo pamoja na wafanyakazi wenzangu wote wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na taasisi zake kwa kuendelea kujituma kwa juhudi na maarifa katika kutekeleza malengo na majukumu ya Afisi yetu. Niwaombe tuendelee kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku na kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na utoaji wa haki kwa wakati.

142. **Mheshimiwa Spika,** kipekee tunawashukuru wahusika wote wa Sekta ya Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao wametupatia ushirikiano wa kutosha katika kuendeleza sekta hii. Shukurani zangu za pekee nazitoa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wote kwa kuchapa vizuri hotuba hii.

## F. HITIMISHO

143. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki cha utekelezaji Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imetekeleza majukumu yake ya msingi kwa kuzingatia Bajeti na Mpango kazi wa Afisi wa mwaka 2021/2022, Sera, Sheria na miongozo mbali mbali ya Serikali na kuhakikisha upatikanaji wa haki, maslahi ya watumishi, usimamizi wa utawala bora, maadili ya viongozi wa umma, udhibiti wa vitendo vya rushwa na utoaji wa huduma kwa wananchi yanatekelezwa ipasavyo.

Kwa mwaka **2022/2023**, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora itaendelea kusimamia na kutekeleza majukumu yake yote hayo muhimu katika uendeshaji wa nchi yetu, kuimarisha utawala bora na upatikanaji wa haki kwa wakati ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Sheria, Utumishi na Utawala Bora inaendelea kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa demokrasia na uchumi wa nchi yetu.

